TANGAZO LA SERIKALI NA. 848 la tarehe 17/11/2023

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA,

(SURA YA 272)

# AMRI

*(Imetolewa kwa mujibu wa kifungu cha 29 (d))*

AMRI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MAFINGA (MAFINGA WSSA), YA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA MWAKA, 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mafinga (Mafinga WSSA), ya Kurekebisha Bei za Huduma za Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2023.

Marekebisho ya bei

2. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Mafinga WSSA zinarekebishwa kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Masharti

3. Bei zilizoidhinishwa zitakuwa na masharti yafuatayo:

(a) kabla ya kutoa bili ya kwanza yenye bei na ada mpya zilizoidhinishwa, Mafinga WSSA itawasilisha ushaidi EWURA wa kuwa imewajulisha wateja wake kuhusu Amri hii na pia imetoa elimu kwa wadau wake ikiwemo wateja, viongozi wa serikali, viongozi wa kisiasa, na wawakilishi wa taasisi za dini juu ya utekelezaji wa Amri ya bei mpya;

(b) ifikapo tarehe 31 Disemba, 2023 au kabla, Mafinga WSSA itawasilisha EWURA mpango wake wa biashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa kiutekelezaji wa masharti ya Amri hii;

(c) Mafinga WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili;

(d) Mafinga WSSA itaandaa na kutekeleza mpango wa kutoa elimu kwa wateja wake na kuwasilisha

EWURA taarifa ya utekelezaji wa mpango huo kila mwaka;

(e) Mafinga WSSA, itahakikisha inafikia viashiria vya utendaji vilivyoainishwa kwenye Jedwali la Tatu;

(f) Mafinga WSSA kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Amri hiii na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Nne;

(g) Mafinga WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa mahitaji ya EWURA, ambazo zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Mafinga WSSA ikilinganishwa na mamlaka nyingine za majisafi na usafi wa mazingira na uboreshaji wa huduma zake; na

(h) kuhakikisha kunakuwepo na huduma endelevu ya maji hususani kipindi cha kiangazi, Mafinga WSSA inapaswa kuandaa na kutekeleza mpango wa kuvuna maji ya mvua.

Kufuta TS Na. 016-12 la Mwaka 2012

4. Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mafinga (Mafinga WSSA), ya Kurekebisha Bei za Huduma za Maji ya Mwaka 2012 imefutwa.

## MAJEDWALI

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

BEI NA ADA ZILIZOIDHINISHWA

1(a): BEI ZA MAJI ZA SASA NA ZILIZOIDHINISHWA

| Kundi la Wateja | Kipimo | Bei ya Sasa | Bei Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | Sh./m3 | 790 | 1,190 | 1,260 | 1,260 |
| Taasisi | Sh./m3 | 880 | 1,250 | 1,320 | 1,330 |
| Biashara | Sh./m3 | 830 | 1,330 | 1,400 | 1,410 |
| Viwanda | Sh./m3 | 930 | 1,400 | 1,480 | 1,490 |
| Magati | Sh./m3 | 500 | 1,000 | 1,000 | 1,000 |
| Wastani wa Bei | Sh./m3 | 786 | 1,190 | 1,250 | 1,260 |

**1(**b): ADA ZA SASA NA ZILIZOIDHINISHWA KWA AJILI YA MAUNGANISHO MAPYA YA MAJI (SHILINGI KWA MAUNGANISHO)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | 32,000 | 26,000 | | |
| Taasisi | 40,000 | | | |
| Biashara | 40,000 | | | |
| Viwanda | 45,000 | | | |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(c))*

MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA

| Na. | KAZI ZITAKAZOTEKELEZWA | GHARAMA (SHS) | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Kununua jumla ya Mita/Dira 300 za Maji za Majumbani za Malipo ya kabla; 120 mwaka 2024/25 na 180 mwaka 2025/26 | | 43,200,000 | 68,040,000 |
| 2. | Kununua jumla ya Mita/Dira 600 za Maji za Majumbani za Malipo ya baada; 200 mwaka 2023/24,100 mwaka 2024/25 na 300 mwaka 2025/26 | 24,000,000 | 12,600,000 | 37,800,000 |
| 3. | Manunuzi ya dira kubwa tatu (3) za maji kwa ajili ya matanki ya maji ya Sabasaba, NSSF, na Posta | | | 4,500,000 |
| 4. | Ujenzi wa Maabara ndogo katika eneo la Mamlaka ya maji Mafinga WSSA | 10,000,000 | | |
| 5. | Ununuzi na ufungaji wa dira mpya na kubwa za maji 12; 2 mwaka 2023/24; 5 mwaka 2024/25 na 5 mwaka 2025/26 | 2,000,000 | 5,250,000 | 5,510,000 |
| 6. | Ujenzi wa jengo la ofisi | | 150,000,000 | 100,000,000 |
| 7. | Ununuzi wa pikipiki 12 new; 7 mwaka 2024/25 na 5 mwaka 2025/26 | | 35,000,000 | 26,250,000 |
| 8. | Ununuzi wa kompyuta mpakato 7 | | | 21,000,000 |
| 9. | Ununuzi wa viti vya ofisi vitano (5); 2 mwaka 2023/24 na 3 mwaka 2025/26 | 1,000,000 | | 1,500,000 |

| Na. | KAZI ZITAKAZOTEKELEZWA | GHARAMA (SHS) | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 10. | Ununuzi wa simu janja mbili (2) | | | 2,000,000 |
| 11. | Ukarabati wa tanki la maji la matofali la Sabasaba lenye ukubwa wa mita za ujazo 135 mwaka 2025/26 | | | 70,000,000 |
| 12. | Ukarabati wa tanki la maji la Posta lenye ukubwa wa mita za ujazo 90 mwaka 2025/26 | | | 20,000,000 |
| 13. | Ujenzi wa uzio kuzunguka tanki la maji posta ujazo wa lenye ukumbwa wa mita za ujazo 90 mwaka 2024/25 | | 10,000,000 | |
| 14. | Ukarabati wa tanki la maji la NSSF lenye ukubwa wa mita za ujazo 45 mwaka 2024/25 | | 30,000,000 | |
| 15. | Ujenzi wa uzio kuzunguka tanki la maji NSSF katika mwaka wa fedha 2025/26 | | | 10,000,000 |
| 16. | Kubadilisha valvu 10; 2 kwa mwaka 2023/24; 4 kwa mwaka 2024/25 na 4 mwaka 2025/26 | 2,000,000 | 3,000,000 | 4,000,000 |
| 17. | Kubadilisha dira kubwa za maji 3 maeneo ya Chanzo cha maji Mkombwe, Chanagrawe, na tanki la maji Kinyanambo | | | 5,000,000 |
| 18. | Kubadilisha bomba chakavu urefu wa 13.5km maeneo ya Changarawe (6km), Pipeline (1.5km), Mkombwe (2km), Kinyanambo (2km), Mjimwema (1km), Lutheran (1km), zenye ukubwa wa kuazia 63mm hadi 160mm, ambapo,3.5km zitafanyika mwaka 2023/24, 5km mwaka 2024/25 na 5km mwaka 2025/26 | 35,000,000 | 52,500,000 | 55,130,000 |
| 19. | Kubadilisha bomba chakavu za daraja B za wateja urefu wa 6km; 2km kila mwaka kwenye kanda tano (5) za Mjimwema,Pipeline, Mkombwe, Lutheran na kanda ya Changarawe | 12,000,000 | 12,600,000 | 13,230,000 |
| 20. | Kubadilisha dira 35 za malipo ya kabla kwa wateja | 12,600,000 | | |
| 21. | Kubadilisha dira za wateja 1,031 za malipo ya baada; ambapo, 231 zitabadilishwa mwaka 2023/24; 400 mwaka 2024/25 na 400 mwaka 2025/26 | 27,720,000 | 50,400,000 | 52,920,000 |

*Tangazo la Serikali Na. 848 (Linaendelea)*

| Na. | KAZI ZITAKAZOTEKELEZWA | GHARAMA (SHS) | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 22. | Kubadilisha komputa mpakato saba (7) kwa wakuu wa idara;ambapo, 2 zitabadilishwa mwaka 2023/24, 2 mwaka 2024/25 na 3 mwaka 2025/26 | 7,000,000 | 7,400,000 | 11,030,000 |
| 23. | Kubadilisha pikipiki sita (6); ambapo , moja (1) itabadilishwa mwaka 2023/24; 2 mwaka 2024/25 na 3 mwaka 2025/26 | 5,000,000 | 10,500,000 | 15,000,000 |
| 24. | Kubadilisha viti/benchi sita (6) vya wateja | | 2,000,000 | 2,100,000 |
| 25. | Kubadilisha Mtandao wa Mawasiliano TTCL kwa 'National ICT Broadband' (NICTBB) | | | 5,000,000 |
| 26. | Kubadilisha simujanja nne (4) | | | 4,000,000 |
| 27. | Kubadilisha vifaa kumi (10) vya ufundi; 3 mwaka 2023/24; 3 mwaka 2024/25 na 4 mwaka 2025/26 | 3,000,000 | 3,200,000 | 4,200,000 |
| | JUMLA | 144,420,000 | 427,910,000 | 522,230,500 |

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(e))*

VIASHIRIA VYA UTENDAJI

| MAELEZO | Kizio | MALENGO YA UTENDAJI | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Idadi ya Watu Iliyofikiwa na Huduma ya Maji | % | 56.9 | 65 | 80 |
| Idadi ya Wateja Wapya Waliounganishwa | Na. | 200 | 300 | 400 |
| Uzalishaji wa Maji | M3 | 1,254,140 | 1,512,195 | 1,658,195 |
| Kiwango cha Upotevu wa Maji | % | 33 | 25 | 20 |
| Ufungaji wa Dira Maji | % | 100 | 100 | 100 |
| Ufanisi wa Ukusanyaji wa Mapato | % | 95 | 95 | 95 |

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(f))*

MAHITAJI YA FEDHA YALIYOIDHINISHWA

| MAELEZO | KIASI (SHILINGI MILIONI) | | |
|---|---|---|---|
| | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Gharama za Uzalishaji wa Maji | 321.01 | 374.95 | 448.92 |
| Gharama za Usambazaji | 3.50 | 3.68 | 3.86 |
| Gharama za Matengenezo na Matunzo | 54.70 | 52.19 | 61.79 |
| Gharama za Wafanyakazi | 314.77 | 381.32 | 443,20 |
| Gharama za Utawala | 135.45 | 153.67 | 161.36 |
| Gharama za Matangazo ya Biashara | 7.21 | 5.47 | 7.84 |
| Kugharamia Matukio na Misaada | 18.62 | 20.55 | 21.58 |
| Tozo za Benki | 1.15 | 1.20 | 1.25 |
| Jumla ya Gharama za Uendeshaji na Matengenezo | 855.42 | 993.02 | 1,149.81 |
| Uchakavu wa Miundombinu | 103.92 | 181.86 | 255.63 |
| Uwekezaji | 40.5 | 246.05 | 266.60 |
| Jumla ya Mahitaji ya Fedha | 1,000.84 | 1,420.93 | 1,672.04 |
| Ada za Maunganisho Mapya | 5.20 | 7.80 | 10.40 |
| Ada za Kurejesha Huduma kwa Waliokatiwa | 1.50 | 1.35 | 1.20 |
| Mahitaji ya Fedha Kutoka Kwenye Mauzo ya Maji | 994.14 | 1,411.78 | 1,660.44 |

Dodoma,
………………..,2023

JAMES A. MWAINYEKULE
*Mkurugenzi Mkuu*